Learning by Ear 2009
Media & Information. Episode 3
Author: Hope Azeda

# Learning by Ear 2009

## Media & Information

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

**EPISODE 3**

| ***CHARACTERS*** | |
|---|---|
| **Announcer:** | **Male/female** |
| **"Young Junior"** | **Male, 15 years old** |
| **"Sister P."** | **Female, 16 years old** |
| **"Charlie"** | **Male, 18 years old** |
| **"Ezra":** | **Male, 22 years old. Brother to "Young Junior".** |
| **"Mr.T":** | **Male, 30, sound technician** |

## INTRO

Hujambo na karibu kwa makala mengine katika mfululizo wa vipindi vyetu vya "Learning By Ear" "Noa Bongo jenga maisha yako" tukizungumzia sekta ya habari na Vyombo vya habari. Na kukumbusha tu yale yaliyotokea katika

kipindi kilichotangulia, wahusika ambao ni wanahabari chipukizi, wamekubaliana kwa kauli moja kuhusu mradi wa kuanzisha kituo cha redio na wanachohitaji kufanikisha mradi huo.Lakini mbali na hayo pia wamegundua wanachohitaji zaidi ni mafunzo kufikia lengo hili. Mr. T ni fundi wa mitambo na anajaribu kuwaeleza majukumu ya wanahabari . Ungana nasi usikie mambo akatavyokua katika kipindi hiki.

**SCENE ONE**

**At Mr T's studio.**

**SFX Knock knock on the door, door opens**

1. **Sister P:** Hbari gani Mr T.

2. **Mr T:** Njema, karibuni ndani .

3. **Charlie:** Uhhh, mbona giza hapa?... kuna shida gani?

4. **Young J:** Nilidhani tutamaliza kurekodi kanda yetu hivi leo.

5. **Mr T:** Yote yatategemea ni wakati gani umeme utakaporudi. Tatizo la kukatizwa kwa umeme limeanza dakika chache tu zilizopita.

6. **Sister P:** Ni bahati mbaya! Hata mimi nilidhani tutakamaliza kurekodi kanda hii leo na tuanze kupanga tutakavyoizindua. Nilikuwa nimeanza kufikira kuhusu bango kubwa mjini likiwa na maandishi: Dot.Com.Club yazindua Album yake ya kwanza, ***"Dream On".***

7. **Charlie:** Sasa tufanyeje ?

| |
|---|
| **Sfx Knocks into things, sounds of things falling down.** |

8. **Young J:** Mr T, unahitaji kuwa na mtambo wa jenereta wakati umeme unapokatika.

9. **Sister P:** Young J, tusubiri dakika chache na ikiwa uememe haurejea mapema twende tufanye mazoezi kaika kituo cha vijana.

10. **Charlie:** Kwa kweli yanayotokea hapa yamenifanya nitafakari umuhimu wa kuwa na mtambo wa jenereta wakati tunapoenelea na mipango ya kuanzisha kituo chetu cha Redio.Jenereta ni muhimu wakati wote hasa kukiwa na tatizo la umeme.

**11. Sister P:** Ni kweli. Redio yetu haipasi kuwa kama ile ya taifa ambako matangazo yanakatizwa mara kwa mara kutokana na ukosefu wa umeme, na kile unachosikia ni sssssssssssss… kwa muda wa dakika tano hivi kasha matangazo yanarejea hewani, muda kidogo shsssssssssss ……ni aibu .

**12. Charlie:** Hatuwezi kubali hilo litokee katika kituo chetu cha Dot.Com.Fm.

**13. Young J:** Je Mr T, wakati tutakapofungua kituo hicho, ungependa kushirikiana nasi kueperusha hewani "***vitu vikali.***"

**14. Mr T:** La hasha… mimi natosheka na kile ninachofanya hapa.!

**15. Sister P:** Si lazima uwe pale wakati wote, unaweza kuwa na kipindi chako maalum na kufanya mambo!. Tunataka kubadilisha hali livyo na kuondoa ukiritimba wa redio ya taifa ambayo imewachosha watu wengi.

**16. Charlie:** Indapo tungekuwa na redio yetu, tungeweza kucheza muziki wetu na ule unaopendwa na mashabiki wengi. Bila shaka tutakuwa maarufu sana humu nchini na hata nje ya mipaka yetu. Tunao uwezo wa kufanya hivyo na kuleta mabadiliko.

**17. Mr T:** Kweli unapozungumzia uwezo wa vyombo vya habari mimi hufikiria sana suala hilo.

**18. Young J:** Kwa nini ?

**19. Mr T:** Redio au sekta ya habari kwa jumla ni nzuri, lakini inategemea wahusika wenyewe. Kwa hivyo mnapasa kuwajibika wakati mnapofikiria kuanzisha kituo hicho cha redio..

**20. Charlie:** Sasa umeanza kunitisha.

**21. Mr T:** Vyombo vya habari hasa Redio vilikuwa mstari wa mbele wakati wa mauaji ya halaiki nchini Rwanda. Redio ilitumiwa kueneza chuki miongoni mwa raia wa Rwanda, na kuchochea uhasama miongoni mwa majirani. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Kwa hivyo

unapozungumzia uwezo wa vyombo vya habari…..

**22. Sister P:** Ahh,sasa naelewa unachomaanisha Mr T, lakini tunataka kubadilisha kabisa sura ya redio humu nchini . Redio ya Dot.Com.FM itakuwa ya kuburudisha tu kucheza muziki wakati wote, sio redio ya kuchochea uhasama bali redio ya kuhubiri umoja na upende miongoni mwa jami.

**23. Young J:** Ni kweli hatutaki kuandaa vipindi vitakavyowachukiza watu. Tumetosheka na vipindi visivyo na maana kwa mfano wakati mtangazaji anapozungumza na mikrofoni kana kwamba hana uhai.

**24. Charlie:** Na tutahakikisha kwamba redio yetu pia inasikika kwenye mtandao.

**25. Mr T:** Ndoto yenu ni kubwa sana .

**END SCENE.**

**SCENE TWO**

| |
|---|
| **SFX: At the bus station in the evening. There is not a lot of traffic passing, but many people are gathered waiting for the bus. Sister P, Charlie and Young J are among the people waiting. Vehicles come and go.** |

**26. Charlie:** Tumelisubiria hili basi kwa muda wa zaidi ya dakika 30 sasa. Mimi nachukua mambo haya. Saa hii ningekua nimefika nyumbani.

**27. Young J:** Usijali kuhusu basi. Kuna mambo mengi tu tuyonapasa kuzunguma tukipanga mikakti ya kuanzisha kituo chetu cha redio..

**28. Sister P:** Mambo kama yapi, Young J? Au bado hujabadili nia ya kuanzisha gazeti?.

**29. Young J:** Wewe ulinishawishi nitupilie mbali nia ya kuanzisha gazeti na ni kashawishika. Tunachopasa kufikiria sasa hivi namna tutakavyopata mafunzo,kwa mfano , ni tofauti kuwa na wazo zuri kama hilo lakini hakuna hata mmoja wetu ambaye amepata mafunzo ya utangazaj.

**30. Charlie:** Ni kweli, na licha ya hayo, tunataka kituo chetu kiwa nambari moja,kwa utangazaji na hatuwezi kufikia hili bila vifaa bora.

**31. Sister P:** Mbali na hayo tunahitaji mahali pazuri kufanya shughuli hiyo

**2. Young J:** Nadhani hii ni changamoto kubwa kwetu sote

.

**33. Sister P:** Bila shaka ni changamoto, kwa hivyo tunachopasa kufanya hivi sasa ni mikakati ya kufanikisha mambo yote haya. Lazima tuwe na mikakati dhabiti.

**34. Charlie:** Vipi, Sister P?

**35. Sister P:** Nisikilize , mradi tu tuwe na moyo a subra na imni tutafanikiwa katika ndoto yetu.Tunaweza kuanza pole pole, chini kabisa huko mashinani na kisha kuimarisha shughuli zetu. Kwa kuanzia tunaweza kununua vifaa kuu kuu na kukodisha chumba kidogo tu. Babu yangu alikuwa akiniambia kuwa

majimbi wanaowika hivi sasa wakati mmoja walikuwa mayai.

**SFX Sound of bus approaching.**

**36. Young J:** Sipendi mafumbo.Ahhha basi ndilo hili limeja, natumai halitaharibikia njiani. Sister P, chunga mkoba wako usijeporwa.

**SFX Bus drives up and stops.**

**END SCENE**

**SCENE THREE**

**SFX On the bus, noisy**

**37. Charlie:** Tuko karibu kufika kituoni .Mbali na muziki tuliourekodi hivi leo, na yote tuliojadiliana, tumekubaliana nini kuhusu mradi wetu wa kuanzisha kituo hicho cha redio?

**38. Sister P:** Kulingana na ule ujuzi kidogo nilionao kuhusu biashara, muhimu ni kupata leseni kutoka kwa halmashauri inayosimamia vyombo vya habari,.. au mwasemaje Charlie?

**39. Charlie:** Kweli Sister P. Nadhani haitakuwa vigumu kupata leseni hiyo.

**40. Young J:** Kwanini unasema hivyo, kwani umewahi kutuma maombi hapo mbeleni?

**41. Charlie:** La hasha, …..aaah lakini tuna mtaalam wa kuandika barua za maombi hapa.

**42. Sister P:** Nani huyo? Kwa kuzinti hli ilivyo ka wakati huu, hatuwezi kugharamia huduma za wataalam.

**43. Charlie:** Sio mtalaam. Namaanisha Young J. nakumbuka tulipokuwa shuleni , Young J alikuwa mwepesi kuwasaidia vijana wengine kuandika barua za mapenzi na hakuna hata mmoja aliyekataa ombi hilo .Tunaweza kutumia ujuzi huo kuandika barua ya maombi ya kutafuta leseni

**44. Young J:** Charlie, tuache utani!.

**45. Sister P:** Ni kweli, si mzaha, tunazungumzia suala la umuhimu mkubwa hapa.

**46. Young J:** Lakini bado nina swali. Sisi hatuna ujuzi wa kutosha kuhusu masuala ya habari, sijui labda ndugu yetu Ezra? Yeye anasomea taaluma hii ya uandishi wa habari katika chuo kikuu cha kitaifa, na pili yeye pia hufanya kazi katika kituo cha redio chuoni humo.

. **47. Charlie:** Ni kweli kabisa!. Ezra anaweza kuwa msaada mkubwa kwetu sote kwa kutushauri. Na zaidi anaweza kutushauri kuhusu vipi tunaweza kupata mafunzo, vifaa na kadhalika.

**48. Sister P:** Mpigie simu tumuliza kama anawezakutusaidia?

**49. Young J:** Baadaye si saa hii. Hapa kuna makelele ndani ya hili basi .Nitampigia simu nikifika nyumbani. Na… kwa kuanza harakati zetu, kesho tunaweza kwenda katika chuo kikuu kumuona Ezra kama hatakuwa na shughuli nyingi, pia tunaweza kumtafuta mtaalam mwengine kutupa ushauri zaidi.

**50. Charlie:** (**Excited).** Nakubaliana nawe, Young J. Kesho twende kumuona Ezra chuoni ... ***Tupa mpampapa, tupa.***

**END EPISODE 3**

**OUTRO**

Huku mpango huo ukianza kushika kasi hatuna budi kukomea hapo kwa leo hadi wakati mwengine.Lakini je ni ushauri gani utakaotolewa na Ezra? Atawahimiza ndugu zake wadogo na rafikize kuhusu suala hili ? Ungana nasi katika makala yajayo tusikie mambo yatakavyokuwa katika mfululizo wa vipindi hivi vya Leaning By Ear .Pia ukipenda unaweza kusikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa Dw- world.de/l b e.

Ukiwa na maoni usisite kututumia.Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa!